TANGAZO LA SERIKALI NA. 835 la tarehe 2/10/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI ZA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA ZA MWAKA 2020

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Jina

1 Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za mwaka 2020.

Eneo la kutumika

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo;

"Afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"daftari la wageni" maana yake ni kitabu maalumu kilichoandaliwa na Mmiliki au kilicho nunuliwa kwa lengo la kusajiri na kutunza kumbukumbu za Wageni wanaolala kwenye nyumba ya kulala Wageni au Hoteli.

"hoteli" maana yake ni nyumba lililojengwa kwa ajiri ya kupokea Wageni au Wasafiri kwa lengo la kujipatia faida na haitajumuisha nyumba yenye vyumba chini ya 6 pia halitajumuisha Mabweni na Nyumba za mapumziko za Serikali;

“Mkurugenzi” maana yake” ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“mgeni” maana yake ni mtu yeyote ambaye hulipa pango la kukaa kwenye Chumba cha nyumba ya kulala wageni kwa siku nzima;

“mmiliki” maana yake ni mtu yeyote anayemiliki na kuendesha biashara ya hoteli au nyumba ya kulala wageni

mtunza Hoteli” maana yake ni mtu yeyote aliyeachiwa jukumu na Mmiliki la kusimamia shughuli za hoteli au nyumba ya kulala wageni za kila siku.

“nyumba ya kulala wageni” maana yake ni Jengo lililo jengwa kwa ajili ya wasafiri na wageni kwa lengo la kupata faida ambayo itajumuisha jengo ambalo lina vyumba vya kulala Wageni chini ya 10 au jengo linaweza kutoa huduma ya Vyumba vya kulala. Tafsiri hii haita jumuisha nyumba za mapumziko za serikali;

“siku” maana yake kipindi cha masaa ishirini na nne baada ya usiku wa manane na kumalizika usiku wa manane unao fuata;

“ushuru wa nyumba ya kulala wageni” maana yake ni kiasi cha fedha kinacho takiwa kulipwa na mmiliki wa Hoteli au nyumba ya kulala wageni kwa Halmashauri;

## SEHEMU YA PILI
## UTOZAJI WA USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI / HOTELI

Kiwango cha ushuru

4 Kila mtunza Hoteli au Mmiliki wa Nyumba ya kulala Wageni au Hoteli atalazimika kulipa Ushuru wa Nyumba za kulala Wageni kwa Halmashauri, ushuru ambao utakuwa sawa na asilimia kumi (10%) ya mauzo ya kila Chumba cha kulala wageni.

## SEHEMU YA TATU
## UKAGUZI KWENYE NYUMBA ZA KULALA WAGENI

Uwezo wa Afisa mwidhiniwa kukagua

5 Afisa Mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa;-

(1) kukagua nyumba ya kulala wageni au hoteli kwa lengo la kutaka kujua kama wageni wote wameingizwa au wamesajiliwa kwenye daftari la wageni;

(2) kukagua kama Mmiliki au mtunza Hoteli ana vitabu halali vya kusajili wageni;

(3) kukagua kama nyumba ya kulala wageni ipo katika hali ya usafi takiwa;

(4) kukagua kama kwenye nyumba ya wageni kuna mahitaji yote yanayo takiwa kuwepo kwenye nyumba ya kulala wageni;

(5) kukagua kama taratibu za kulaza wageni kwenye nyumba ya kulala wageni zinafuatwa.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA KULAZA WAGENI KWENYE NYUMBA YA KULALA WAGENI/ HOTELI

Masharti ya kutunza hoteli

6 Kila Mmiliki au mtunza hoteli au nyumba ya kulala Wageni atahakikisha yafuatayo yanatekelezwa au yanafanyika:-

(a) Kila mgeni anasajiliwa kwenye daftari la kulala wageni kwa kuingiza taarifa zote muhimu bila kujali muda aliokitumia chumba ;
(b) Kulipa Ushuru wa Nyumba ya kulala Wageni kwa Halmashauri ndani ya siku 15 baada ya mwezi husika wa mauzo;
(c) Kulipa ada ya leseni ya biashara ya nyumba ya kulala wageni ndani ya muda uliowekwa kwa mujibu wa Sheria;
(d) Kuhakikisha kuwa nyumba ya kulala Wageni inakuwa safi muda wote na masharti mengine ya usafi yanafuatwa.
(e) Kuweka wazi vitabu vya kumbukumbu vya wageni na nyaraka zingine wakati wa ukaguzi; na
(f) Kuhakikisha kuwa biashara ya nyumba za kulala Wageni inakuwa na leseni itakayowekwa wazi eneo la Biashara na kuzingatia masharti yote kama yalivyo fafanuliwa kwenye Sheria ya leseni na miongozo ya biashara.

## SEHEMU YA TANO
## ULINZI WA MALI ZA MGENI NA HUDUMA ZA LAZIMA KWA MGENI

Wajibu wa mmiliki

7 Itakuwa ni jukumu la kila Mmiliki wa Nyumba ya kulala Wageni kuhakikisha kuwa:

(a) Kunakuwa na ulinzi wa kutosha wa mgeni na mali zake na milango na madirisha imara;
(b) Kwenye kila chumba cha kulala mgeni yanatolewa mahitaji yote ya msingi ambayo ni sabuni ya kuogea, mswaki, dawa ya meno, kondomu, maji ya moto, taulo, mashuka na mahitaji mengine mhimu kwa mgeni yanakuwa katika hali ya usafi; na
(c) Kutoa stakabadhi kwa mgeni baada ya kupokea malipo.

## SEHEMU YA SITA
## ADHABU

Adhabu

8 Mtu yeyote atakaye kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/= na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo

Kufililisha

9. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama ilivyoekelezwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hizi.

## JEDWALI

(*Limetungwa* chini *ya Kifungu cha 9*)

## HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ………………………………………………… nakiri mbele ya ………………………………… ambaye ni Mkurugenzi, kwamba, mnamo tarehe ……. ya mwezi ……… mwaka ………… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ………… cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa nyumba za Kulala wageni) za Halmashauri ya Jiji la Mbeya za mwaka 2020.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kwa hiyari yangu niko tayari kulipa kiasi cha ushuru wa nyumba za Kulala wageni unaodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu na ufahamu wangu.

Leo tarehe …… ya mwezi …………… mwaka …………
Jina……………………..…………………………
Saini……………

Mbele ya:
Jina………………………………………………….
Cheo ……………………………………………..
Saini ………………

Muhuri wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa azimio la kikao cha Mkuatano wa baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 10/06/2020 na kubandikwa mbele ya;

SAAD A. MTAMBULE
*Kaimu Mkurugenzi*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

**LS**

GIBSON J. MWAKALIBULE
*Mwenyekiti wa Mkutano*
*Halmashauri ya Jiji la Mbeya*

**NAKUBALI**

DODOMA
05 Agosti, 2020

SELEMANI S. JAFO
WN OR-TAMISEMI
**DODOMA**